# WILAYA YA BUSIA

# DARASA LA TANO MUHULA WA TATU

PENPLUS BUSIA

# KISWAHILI

*Muda: Saa 1 Dakika 40*

***Jaza nafasi wazi***

Mlango __1__ mwalimu __2__ Kiswahili __3__ alikuwa wa __4__ kuingia katika darasa __5__ la tano. Kipindi __6__ asubuhi kilikuwa __7__. Alitusabahi kama __8__ desturi __9__. Baada ya shughuli ndogo ndogo za hapa na pale __10__ darasani, alianza kutuelezea __11__ kuandika hati safi __12__ darasani, __13__ pia maishani __14__. Kisha alituita __15__ ubaoni tukaandika neno HATI.

1. A. ulipofunguliwa B. ulipofungwa
   C. ulipofungulia D. ulifunguliwa
2. A. ya B. wa C. cha D. kwa
3. A. ndio B. ndiyo C. ndiye D. ndivyo
4. A. kuanza B. kwanza C. kuwanza D. kwenda
5. A. yetu B. mwetu C. kwetu D. letu
6. A. kile cha B. ile ya C. hiyo ya D. hii ya
7. A. yake B. chake C. lake D. wake
8. A. aliyokuwa B. lilivyokuwa
   C. ilikuwa D. ilivyokuwa
9. A. yetu B. kwake C. yake D. wetu
10. A. ule B. lile C. zile D. mle
11. A. jinsi ya B. hali ya
    C. vile ya D. ukweli wa
12. A. siko tu B. siyo tu C. sio tu D. sivyo tu
13. A. mbali B. pale C. bali D. vile
14. A. yetu B. mwetu C. zetu D. wetu
15. A. moja B. mmoja
    C. mojawapo D. mmoja mmoja

***Chagua jibu sahihi***

16. "Sango hatakuja." Sentensi hii ni ya wakati upi?
    A. Ujao B. Uliopita C. Uliopo D. Usiojulikana
17. Mwalimu alituletea habari ________
    A. njema B. mwema C. jema D. chema
18. Mkutano ulihudhuriwa na watu wengi sana. Yaani wake ______ wanaume.
    A. kwa B. na C. pa D. pamoja
19. Tumia alama sahihi ya uakifisho. "Kumbe Juma ni mwizi ______
    A. (?) B. (!) C. (") D. (.)
20. Tumia kiashiria kisisitizi kujaza pengo.
    "Nyavu ________ hizo ndizo zangu."
    A. hizo B. hizi C. zizi D. zizo
21. Bonde la ufa: kwa wingi ni:
    A. Bonde za ufa B. Mabonde ya nyufa
    C. Mabonde za nyufa D. Mabonde ya ufa
22. ______ kifupi zaidi huitwa mbilikimo.
    A. Mtu B. Kamtu C. Kimtu D. Kijitu
23. Utiriri, kereng'ende, kiroboto na mavu kwa jina moja ni ______
    A. wanyama B. wadudu C. matunda D. nyuni
24. Watu walitoka uwanjani
    A. mmoja mmoja B. moja moja
    C. mmoja kwa mmoja D. kimoja kimoja
25. Vitabu vyetu ______ nyumbani.
    A. vi B. zi C. yu D. ki

***Tumia "amba" kukamilisha sentensi zifuatazo***

26. Mkeka ________ umenunuliwa ni mzuri.
    A. ambao B. ambazo C. ambaye D. ambayo
27. Kuku ________ walikufa ni wa babu.
    A. ambazo B. ambacho
    C. ambako D. ambao
28. Kuta ________ zimebomoka zitarekebishwa.
    A. ambazo B. ambayo
    C. ambayo D. ambako
29. Kuimba ________ nilikusikia ni kuzuri.
    A. ambaye B. ambao C. ambazo D. ambako
30. Mambo ________ tunayasikia ni mabaya.
    A. ambazo B. ambao C. ambayo D. ambaye

***Soma habari hii kisha ujibu maswali 31-40.***

Vijiji vya wilaya vimebaki kama visiwa na wakazi wote hawawezi kuondoka kwenda mahali popote kwa sababu ya kuzingirwa na mafuriko. Tangu mvua kubwa ianze kunyesha sehemu zote, wananchi hawajapokea misaada yoyote ya usafiri, vyakula wala dawa za kujikinga na kujitibu kutokana na magonjwa kama vile kichocho, malaria, homa ya matumbo na kuhara. Kwa muda mrefu sana mvua kubwa imekuwa ikinyesha katika magatuzi yote ya nchi yetu.

Kulingana na maelezo ya wataalam wa hali ya mazingira, mafuriko hayo yamesababishwa na hatari za kuharibu mazingira kote nchini. Watu wanakata miti ovyo ovyo na kulima kila sehemu. Hawajui kwamba mizizi ya miti hiyo ndiyo inayoshikilia udongo na kuzuia mmomonyoko. Pia watu wengine wanalima hadi kando kando ya mito na kusababisha kuwapo kwa udongo laini karibu na kingo za mto.

Tatizo jingine ni kujenga kila mahali bila kuyajali mazingira. Wakati umefika ambapo lazima tuyatunze mazingira vizuri la sivyo, majanga yatakuwa mengi. Na janga ni jangamizi, huangamiza.

31. Vijiji vimebaki kama visiwa kwa sababu _____
A. ya kuzungukwa na mafuriko
B. wakazi hawawezi kutoka
C. hawajapokea misaada
D. hakuna dawa

32. Tangu mvua ianze kunyesha _________
A. wakazi wamekata miti
B. magonjwa yamezidi
C. hakuna magonjwa
D. wataalam wamekuja

33. Mvua kubwa imekuwa ikinyesha kwenye _______
A. baadhi za wilaya B. vijiji vingine
C. kila gatuzi D. sehemu fulani za nchi

34. Wataalam wa mazingira wanasema _______
A. mafuriko ni hatari
B. watu wanakata miti
C. mvua itazidi
D. uharibifu wa mazingira ni hatari

35. Mizizi ya miti _________
A. husaidia kushikilia udongo usimomonyoke
B. husababisha mafuriko karibu na mito
C. husababisha udongo kuwa laini
D. ni dawa ya tumbo

36. Tunaambiwa kwamba watu wengine wanalima _____
A. kwenye mito B. Karibu sana na mito
C. mazingira ya mto D. kutoa mizizi

37. Tuyatunze mazingira ili ______
A. tujenge mbali na mto
B. kuzuia udongo usimomonyoke
C. kuleta janga la mafuriko
D. tusilime

38. Mara nyingi mafuriko hutokea nyakati za _____
A. masika B. kiangazi
C. vuli D. kipupwe

39. Katika taarifa hii neno "wakazi" lina maana ya watu ambao _________
A. ni wafanyakazi B. wana kazi
C. ni wenyeji D. ni wa kazi

40. Taarifa hii ni kuhusu janga la _______
A. mazingira B. mafuriko
C. miti D. magonjwa

***Soma kisa kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50.***

Ulevi una vituko vyake. Sugu na Sungu walikuwa na mazoea ya kunywa pombe pamoja. Sugu alikuwa mlevi kuliko Sungu. Lakini ulevi ni ulevi tu hata ukinywa kidogo wewe ni mlevi tu.

Siku moja Sungu alikunywa pombe yake akamaliza. Akasema, "Rafiki yangu Sugu, mimi ninaenda nyumbani, watoto wangu wapo nyumbani wamefunga shule. Naenda nikakae nao ili tuongee!" Aliondoka saa mbili usiku. Alipokuwa akienda alipitia kwenye kichochoro cha katikati ya mahali penye makaburi. Bahati mbaya, Sungu aliteleza akatumbukia ndani ya kaburi lililokuwa wazi. Lilichimbwa ili kumzikia maiti kesho yake. Alipojaribu kutoka alishindwa. Ujanja ukaisha na ulevi ukatoweka.

Usiku saa tano, Sugu naye alianza mwendo kuelekea nyumbani. Usiku saa tano, Sugu naye alianza mwendo kuelekea nyumbani. Alilewa, alipitia kichochoro cha makaburi akiimba nyimbo za ulevi. Kufika pale penye kaburi wazi, alitumbukia ndani kwa kishindo. "Kub!" Alishtuka sana alipomwangukia mtu maiti labda. Pombe ikamtoka akilini. Alijaribu kutoka ili asikae na maiti yule, lakini alishindwa. Akasikia sauti ikisema, "Usijisumbue ndugu yangu, hata mimi nimeshindwa kutoka. Mimi na wewe leo sote tu maiti!"

41. Sugu na Sungu walizoea _______
A. kulewa sana
B. kuuza pombe
C. kunywa pombe gengeni
D. kutembea pamoja

42. Siku moja Sungu _______
A. alilewa sana akaanguka
B. alibaki gengeni
C. alirudi nyumbani mapema
D. alimwacha Sugu gengeni

43. Ni watoto gani waliofunga shule?
A. Watoto wa Sungu B. Watoto wa Sugu
C. Watoto wa gengeni D. Watoto walevi

44. Sungu aliondoka gengeni saa mbili ili aende wapi?
A. Makaburini B. Kichochoroni
C. Kwa maiti D. Kuongea na watoto wake

45. Sungu alipoteleza na kutumbukia kaburini ______
A. alishindwa kutoka B. alipata maiti
C. alimngojea sugu D. alilewa sana

46. Kaburi lililokuwa wazi lilikuwa la kumzikia _______
A. Sugu B. Sungu
C. maiti D. mlevi

47. Kwa nini Sugu alishtuka alipotumbukia kaburini?
A. Alimkuta maiti
B. Alijua amemwangukia maiti
C. Alimwona Sungu
D. Alilewa sana

48. Sauti ambayo Sugu aliisikia kaburini ilikuwa ya ___
A. Sungu B. Maiti C. Shetani D. Mlevi

49. Mwishowe kwa maoni yako, unadhani vipi?
A. Walevi na maiti wote ni sawa
B. Maiti na walevi wote wanapendana
C. Sugu na Sungu wote walilala kaburini usiku kucha
D. Walevi wote wawili walitoka kaburini usiku huo huo

50. Kichwa kisichofaa habari hii ni _______
A. Vituko vya walevi B. Kaburi la walevi
C. Walevi na maiti D. Ulevi na hatari